

WATUMISHI 73 WAPANDISHWA VYEO KATIKA TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

Watumishi 73 wamepandishwa vyeo kutokana na sifa na utendaji wa kazi wenye matokeo mazuri na tija katika Utumishi wa Umma.

Zoezi hilo limefanyika mwanzoni mwa Januari, 2010, baada ya Tume ya Utumishi wa Umma kuainisha na kutenga nafasi za watumishi waliostahili kupandishwa vyeo na kutenga fedha za kulipa mishahara mipya kwa ajili ya watumishi hao.

Nafasi zilizotengwa kwa ajili ya watumishi kupandishwa vyeo ni 105. Lakini watumishi ambao tayari wamepandishwa ni 73.

Katika nafasi 3 za Afisa Rasilimali Watu Mkuu II, nafasi hizo zimejazwa na watumishi 3, nafasi ya Afisa Ugavi Mkuu I, nafasi hiyo imejazwa na mtumishi 1, nafasi 3 za Afisa Tawala Mwandamizi, lakini nafasi 1 tu imejazwa, nafasi 22 za Maafisa Elimu Wasaidizi Waandamizi, zimejazwa nafasi 21, nafasi 1 ya Mhasibu Mwandamizi imejazwa na mtumishi 1, nafasi 2 za Watunza Kumbukumbu Wasaidizi Waandamizi zimejazwa na watumishi 2, nafasi 11 za Maafisa Wasaidizi, lakini mtumishi 1 tu ndio aliyejaza nafasi hiyo.

Aidha, nafasi 2 za Wachambuzi wa Mifumo ya Kompyuta, nafasi hizo zimejazwa, nafasi 27 za Watunza Kumbukumbu I zimejazwa nafasi 22, nafasi 5 za Katibu Mahususi I zimejazwa nafasi 4, nafasi 24 za Katibu Mahususi zimejazwa nafasi 12 na nafasi 4 za madereva zimejazwa nafasi 3.

Upandishwaji vyeo katika utumishi wa umma unazingatia sera ya Menejimenti katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999 na Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebisha na Sheria Na. 18 ya mwaka 2007. katika sheria hiyo, kigezo kikuu cha kupandishwa vyeo watumishi ni sifa. Kama msimamizi wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 kuona kama inazingatiwa ipasavyo na Mamlaka ya Ajira na Nidhamu na waajiri katika Utumishi

wa Umma, Tume ya Utumishi wa Umma imezingatia vigezo vyote vilivyotakiwa katika nafasi mbalimbali zilizojazwa.

Zoezi la kupandishwa vyeo watumishi katika Tume ya Utumishi wa Umma litaendelea tena katika robo ya III ya mwaka wa fedha 2009/2010.

Tume ya Utumishi wa Umma inachukua fursa hii pia kuwakumbusha waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002, kanuni na taratibu zake za mwaka 2003 wakati wa kuendesha masuala ya kiutumishi ili kuhakikisha kuwa haki inatendeka kwa kila mtumishi.

Iwapo una maoni/maswali tafadhali tuandikie,

**Katibu,
Ofisi ya Rais,
Tume ya Utumishi wa Umma,
S.L.P. 9143,
DAR ES SALAAM.**